MAGAZETI-NOVEMBA 6, 2026

1. UHURU NOV 6, 2026

Mchakato wa Katiba mpya unaendelea - Dk. Mwigulu

DODOMA
Na FRED ALFRED

WAZIRI Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema maandalizi ya mchakato wa upatikanaji katiba mpya yanaendelea kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na utaratibu wa kisheria.

Amesema baada ya maandalizi hayo kukamilika, Bunge na Watanzania watajulishwa.

Amesisitiza kuwa, serikali inalipa uzito suala hilo na kwamba miongoni mwa hatua zilizoanza kuchukuliwa ni kufuata utaratibu wa kisheria utakaowezesha mchakato huo kuendeshwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Dk. Mwigulu aliyasema hayo bungeni jijini hapa, jana, alipojibu swali la Mbunge wa Tunduru Kaskazini (ACT - Wazalendo), Ado Shaibu, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kuhusu utekelezaji wa ahadi ya kufufua mchakato wa katiba mpya, lini utaanza na utakuwa na sura gani.

Ado katika swali lake, alisema amekuwa akihoji ndani ya Bunge kuhusu utekelezaji ahadi hiyo, huku mawaziri mbalimbali wakilihakikishia Bunge kwamba nia ya serikali kufufua mchakato wa katiba mpya ipo palepale.

"Bunge la sasa linakaribia kutimiza mwaka mmoja tangu kuzinduliwa rasmi Novemba mwaka jana, Watanzania wanahitaji kupata ufafanuzi zaidi kuhusu hatima ya mchakato huo," alisisitiza.

Hivyo, alimuomba waziri mkuu ambaye ndiye mwenye dhamana ya kuratibu shughuli za serikali ndani ya Bunge, kutoa kauli itakayowapa Watanzania matumaini kuhusu lini mchakato huo utaanza na utaratibu utakaotumika.

Akijibu swali hilo, Dk. Mwigulu alisema serikali imetoa matamko mara kadhaa kuhusu suala hilo kutokana na umuhimu wake kwa taifa.

Dk. Mwigulu alisema suala la katiba mpya limepewa uzito na serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia na siyo jambo lililobaki katika kauli pekee, bali limejumuishwa ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aliongeza kuwa, suala hilo lilijadiliwa katika vikao mbalimbali vya Chama chini ya Mwenyekiti wake, Rais Dk. Samia na kukubaliwa kuwa jambo muhimu linalopaswa kutekelezwa.

"Jambo hili la Katiba ni jambo kubwa na serikali chini ya Dk. Samia Suluhu Hassan inalipa uzito. Suala hili halijaishia kwenye maneno tu, kwa uzito wake liliwekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi," alisema.

Vilevile, alisema Rais Dk. Samia alipokuwa akizindua Bunge alieleza mambo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi yatatekelezwa, huku akitoa mwongozo utakaotumika kutekeleza mchakato huo.

Dk. Mwigulu alisema pamoja na mwongozo huo, upo utaratibu wa kisheria unaopaswa kufuatwa ikiwemo kufanya marekebisho ya sheria, yatakayowezesha kuanza na kuendesha mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

Alisema hatua hizo zinaendelea na baada ya kukamilika kwa maandalizi yote ya kisheria yakiwemo marekebisho ya sheria husika, Bunge na Watanzania watajulishwa.

"Zitakapokuwa zimekamilika yakiwemo marekebisho ya sheria kuongoza utaratibu huo kwa mujibu wa sheria, Bunge lako tukufu litajulishwa na Watanzania watajulishwa," alisisitiza.

Alisisitiza kuwa, serikali inatambua Katiba ni sheria mama na msingi wa utawala wa sheria, utawala bora, uwajibikaji na upatikanaji wa haki, hivyo ni muhimu kufuata utaratibu ili kupata Katiba itakayokuwa na manufaa kwa taifa kwa miaka mingi ijayo.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha mchakato huo unafanyika kwa utaratibu unaozingatia misingi ya sheria, kulinda amani na utulivu uliopo nchini.

CamScanner

1. UHURU NOV 6, 2026

HOJA YA HAJA

Katika eneo la demokrasia na ushiriki wa wananchi, Tanzania imeeleza hatua zilizochukuliwa kupitia mazungumzo ya kitaifa na wadau wa vyama vya siasa yaliyoendeshwa na Kikosi Kazi kuhusu Demokrasia ya Vyama Vingi.

Tanzania yaweka bayana mafanikio ya haki za binadamu UN

Na MWANDISHI WETU

TANZANIA imewasilisha hatua na mafanikio mbalimbali iliyoyapata katika kuimarisha ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu, ikieleza mageuzi yaliyofanyika katika sekta ya sheria na haki, demokrasia, utawala bora, usawa wa kijinsia na upatikanaji wa huduma za kijamii.

Mafanikio hayo yamewasilishwa katika Kikao cha Nne cha Tathmini ya Hali ya Haki za Binadamu kwa Mataifa (Universal Periodic Review - UPR), kinachofanyika katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa jijini Geneva, Uswisi.

Katika wasilisho hilo lililofanyika Novemba 5, 2026, Tanzania imeeleza hatua mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha tathmini, huku ikisisitiza dhamira ya Serikali ya kuendelea kuimarisha taasisi na mifumo ya utoaji haki pamoja na kulinda utu wa kila mtu kwa kuzingatia Katiba, sheria za nchi na wajibu wa kimataifa kuhusu haki za binadamu.

Ripoti hiyo imeeleza kuwa katika tathmini iliyopita ya mwaka 2021, Tanzania ilipokea jumla ya mapendekezo 252 kutoka kwa nchi mbalimbali, ambapo ilikubali mapendekezo 187, yakiwamo 20 yaliyokubaliwa kwa sehemu, huku 65 yakikataliwa.

Mapendekezo yaliyokubaliwa yamekuwa sehemu ya msingi wa mageuzi na hatua mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha taarifa.

Katika eneo la upatikanaji wa haki, Tanzania imeeleza mafanikio yaliyopatikana kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, ambayo imewafikia takribani wananchi milioni 7.9, wakiwamo wanawake zaidi ya milioni nne.

Kampeni hiyo inalenga kuwawezesha wananchi kupata huduma za kisheria na kuondoa vikwazo vinavyotokana na gharama, umbali na ukosefu wa uelewa kuhusu masuala ya sheria.

Aidha, Serikali imefanikiwa kutafsiri sheria 446 kwa lugha ya Kiswahili ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za kisheria na kuwawezesha wananchi kuelewa haki na wajibu wao.

Katika kuimarisha utendaji wa Mahakama, Tanzania Bara imepunguza mrundikano wa mashauri kutoka takribani asilimia 10 hadi asilimia tano, huku muda wa wastani wa kumaliza mashauri ukipungua kutoka siku 95 hadi 66.

Kwa upande wa Zanzibar, mrundikano wa mashauri umepungua kutoka asilimia 43 hadi asilimia 18.

Vilevile, matumizi ya teknolojia katika utoaji haki yamewezesha kuhitimishwa kwa mashauri zaidi ya 170,000 kupitia mifumo ya mahakama za kidijitali na vikao vya mtandaoni.

Kwa sasa, magereza 66 yana huduma za kuunganishwa na Mahakama kwa njia ya mtandao, hatua inayolenga kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wafungwa na mahabusu.

Katika eneo la demokrasia na ushiriki wa wananchi, Tanzania imeeleza hatua zilizochukuliwa kupitia mazungumzo ya kitaifa na wadau wa vyama vya siasa yaliyoendeshwa na Kikosi Kazi kuhusu Demokrasia ya Vyama Vingi.

Mazungumzo hayo yalichangia kuondolewa kwa zuio la mikutano ya hadhara ya kisiasa na kurejeshwa kwa vibali vya magazeti manne yaliyokuwa yamesimamishwa.

Aidha, mageuzi ya sheria za uchaguzi yamejumuisha kuweka utaratibu wa uwazi katika upatikanaji wa baadhi ya makamishna wa uchaguzi kupitia maombi, uchujaji na usaili.

Mageuzi hayo pia yameweka sharti la wagombea wa ubunge na udiwani wasiokuwa na wapinzani kupata ridhaa ya wapiga kura kupitia utaratibu wa kupigiwa kura.

ENZI HIZO



WAZIRI Mkuu, Ndugu Rashidi Kawawa (wa pili kulia), akishiriki ujenzi wa nyumba, katika Kijiji cha Ujamaa Mvuti, Wilaya ya Ilala mkoani Dar es Salaam, Hiyo ilikuwa Novemba 20, 1976

CamScanner

2. MWANANCHI NOV. 6, 2026



Tanzania yatoa taarifa ya haki za binadamu Umoja Mataifa

UK 3

Wanayojiuliza wanawake kuhusu afya

Ni maswali ambayo daktari anayapokea kila wiki kutoka kwa wanawake ambao wana-hofia kimyakimya mambo waliyosoma kwenye... UK 12

SUPA JACKPOT
TZS. 1,393,159,889
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

MWANANCHI

TANZANIA

Ijumaa, Novemba 6, 2026 MWANANCHI.CO.TZ ISSN 0856-7573 NA. 9581 BEI: TSH 1,000, KSH 60

CamScanner

2. MWANANCHI NOV. 6, 2026

Tanzania yatoa taarifa ya haki za binadamu UN

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Geneva. Tanzania imeeleza hatua na mageuzi iliyotekeleza katika kuimarisha haki za binadamu, ikiwamo kuwafikishia wananchi milioni 7.9 huduma za msaada wa kisheria, kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani na kupanua matumizi ya teknolojia katika utoaji haki.

Mafanikio hayo yamewasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Abdallah Ulega katika Kikao cha Nne cha Tathmini ya Hali ya Haki za Binadamu kwa Mataifa (Universal Periodic Review – UPR), kinachofanyika chini ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, jijini Geneva, Uswisi.

Katika wasilisho hilo la Novemba 5, 2026, Serikali imeeleza mageuzi yaliyofanyika katika sekta ya sheria na haki, demokrasia, utawala bora, usawa wa kijinsia na upatikanaji wa huduma za kijamii.

Tanzania imesisitiza dhamira yake ya kuendelea kuimarisha taasisi na mifumo ya utoaji haki, pamoja na kulinda utu wa kila mtu kwa kuzingatia Katiba, sheria za nchi na wajibu wake wa kimataifa katika masuala ya haki za binadamu.

Katika kuimarisha ufanisi wa mfumo wa utoaji haki, Tanzania Bara imeeleza kupungua kwa mrundikano wa mashauri mahakamani kutoka takribani asilimia 10 hadi asilimia tano.

Pia, muda wa wastani wa kumaliza mashauri umepungua kutoka siku 95 hadi siku 66, hatua inayoashiria kuimarika kwa kasi ya usikilizaji na utatuzi wa mashauri.

Kwa upande wa Zanzibar, mrundikano wa mashauri umepungua kutoka asilimia 43 hadi asilimia 18.

Mafanikio mengine yaliyowasilishwa yanahusu matumizi ya teknolojia katika utoaji haki, ambapo mashauri zaidi ya 170,000 yamehitimishwa kupitia mifumo ya mahakama za kidijitali na vikao vinavyofanyika kwa njia ya mtandao.

Aidha, magereza 66 tayari yameunganishwa na Mahakama kupitia huduma za mtandao, hatua inayorahisisha upatikanaji wa huduma za kimahakama kwa wafungwa na mahabusu.

Katika eneo la demokrasia na ushiriki wa wananchi, Serikali imeeleza hatua zilizochukuliwa kupitia mazungumzo ya kitaifa na wadau wa vyama vya siasa, yaliyofanywa na kikosi kazi kuhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Mazungumzo hayo yalichangia kuondolewa kwa zuio la mikutano ya hadhara ya kisiasa na kurejeshwa kwa vibali vya magazeti manne yaliyokuwa yamesimamishwa.

Hatua hizo zimetajwa kama sehemu ya jitihada za kuboresha mazingira ya ushiriki wa kisiasa na kupanua nafasi ya wadau mbalimbali kushiriki katika shughuli za kidemokrasia.

Pia, Serikali iliieleza mageuzi ya sheria za uchaguzi yaliyohusisha kuweka utaratibu wa uwazi katika upatikanaji wa baadhi ya makamishna wa uchaguzi.

Utaratibu huo unahusisha kupokea maombi, kufanya uchujaji na usaili wa waombaji, hatua inayolenga kuimarisha uwazi katika mchakato wa kuwateua viongozi hao.

Mageuzi mengine ni kuweka sharti la wagombea wa ubunge na udiwani wasiokuwa na wapinzani kupata ridhaa ya wapigakura.

Katika wasilisho hilo, Tanzania pia imeeleza namna ilivyotekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika tathmini iliyopita ya mwaka 2021.

Katika tathmini hiyo, nchi ilipokea jumla ya mapendekezo 252 kutoka kwa mataifa mbalimbali, ambapo iliikubali mapendekezo 187, yakiwamo 20 yaliyokubaliwa kwa sehemu, huku 65 yakikataliwa.

Serikali ilisema mapendekezo yaliyokubaliwa yamekuwa msingi wa mageuzi na hatua mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi cha taarifa.

CamScanner



Waziri wa Katiba na Sheria, Abdallah Ulega akiwasilisha taarifa ya mafanikio na hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Tanzania katika kuimarisha ulinzi na utekelezaji wa Haki za Binadamu, wakati wa Kikao cha 53 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kinachofanyika Geneva, Uswisi jana. Kushoto ni Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Ofisi za Umoja wa Mataifa, Dk Abdallah Possi. (Picha na Wizara ya Sheria na Katiba).

Tanzania yaanika mafanikio, mageuzi haki za binadamu

Na Mwandishi Maalumu, Geneva

TANZANIA imeeleza mafanikio yaliyopatikana kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Imeeleza hayo wakati ikiwasilisha mafanikio na hatua ilizochukua katika kuimarisha ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu kwenye Kikao cha Nne cha Tathmini ya Hali ya Haki za Binadamu kwa Mataifa kinachofanyika katika Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa jijini Geneva, Uswisi jana.

Katika taarifa hiyo, Tanzania ilieleza mageuzi yaliyofanyika katika sekta ya sheria na haki, demokrasia, utawala bora, usawa wa kijinsia na upatikanaji wa huduma za kijamii.

Ilieleza kampeni hiyo ya msaada wa kisheria imewafikia takribani wananchi milioni 7.9, wakiwamo wanawake zaidi ya milioni nne.

Kampeni hiyo inalenga kuwawezesha wananchi kupata huduma za kisheria na kuondoa vikwazo vinavyotokana na gharama, umbali na ukosefu wa uelewa wa masuala ya sheria.

Serikali imeeleza imefanikiwa kutafsiri sheria 446 kwa Lugha ya Kiswahili ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za kisheria na kuwawezesha wananchi kuelewa haki na wajibu wao.

Ripoti hiyo imeeleza katika tathmini iliyopita mwaka 2021 Tanzania ilipokea mapendekezo 252 kutoka kwa nchi mbalimbali, ilikubali mapendekezo 187 yakiwamo 20 yaliyokubaliwa kwa sehemu, huku mapendekezo 65 hayakukubaliwa.

Mapendekezo yaliyokubaliwa yamekuwa sehemu ya msingi wa mageuzi na hatua zilizotekelezwa katika kipindi cha taarifa.

Katika kuimarisha utendaji wa mahakama, Tanzania Bara imepunguza mrundikano wa mashauri kutoka takribani asilimia 10 hadi asilimia tano, huku muda wa wastani wa kumaliza mashauri ukipungua kutoka siku 95 hadi siku 66.

Kwa upande wa Zanzibar, mrundikano wa mashauri umepungua kutoka asilimia 43 hadi asilimia 18.

Vilevile, matumizi ya teknolojia katika utoaji haki yamewezesha kuhitimishwa kwa mashauri zaidi ya 170,000 kupitia mifumo ya mahakama za kidijiti na vikao vya mtandaoni.

Kwa sasa, magereza 66 yana huduma za kuunganishwa na mahakama kwa njia ya mtandao, hatua inayosaidia kurahisisha upatikanaji wa haki kwa wafungwa na mahabusu.

Katika eneo la demokrasia na ushiriki wa wananchi, Tanzania imeeleza hatua zilizochukuliwa kupitia mazungumzo ya kitaifa na wadau wa vyama vya siasa yaliyofanywa na Kikosikazi kuhusu Demokrasia ya Vyama Vingi, yaliyochangia kuondolewa kwa zuio la mikutano ya hadhara ya kisiasa na kurejeshwa kwa vibali vya magazeti manne yaliyokuwa yamesimamishwa.

CamScanner

4. GAZETI LA DAILY NEWS NOV. 6, 2026

TZ steps up human rights agenda

By DAILY NEWS Reporter

TANZANIA has reported significant progress in strengthening human rights protection, expanding access to justice and improving essential public services, highlighting legal, institutional and socioeconomic reforms undertaken under President Samia Suluhu Hassan.

Presenting the country's record during the Fourth Universal Periodic Review (UPR) before the United Nations Human Rights Council Working Group in Geneva, Constitutional and Legal Affairs Minister Abdallah Ulega (pictured) outlined improvements in judicial efficiency, legal awareness, digital access and social protection.

A major achievement is the Mama Samia Legal Aid Campaign, which has reached approximately 7.9 million people, including more than 4 million women, helping communities overcome financial and geographical barriers to legal assistance.

The government has also translated 446 statutes into Kiswahili to make laws more accessible and enable citizens to understand their rights and responsibilities.

These efforts have been accompanied by improvements in the administration of justice. On Mainland Tanzania, the case backlog declined from approximately 10 per cent to 5 per cent, while the average time required to determine cases fell from 95 days to 66 days.

In Zanzibar, the backlog dropped from 43 per cent to 18 per cent, Ulega said.

Digital systems have further

Continues on Page 3



A major achievement is the Mama Samia Legal Aid Campaign, which has reached approximately 7.9 million people, including more than 4 million women, helping communities overcome financial and geographical barriers to legal assistance.

CamScanner

4. DAILY NEWS NOV. 6, 2026

...with peace among countries in the region. (Photo by Parliament)

TZ steps up human rights agenda

Continued from Page 1

expanded access to justice, with more than 170,000 cases concluded through digital and virtual court arrangements. A total of 66 prisons have virtual court connectivity, while mobile courts operate in four regions. High Courts and appellate courts also conduct virtual hearings.

Beyond the justice sector, Tanzania highlighted investments in education, health care, electricity, water and infrastructure as important elements of its efforts to improve citizens' welfare and advance human rights.

The number of health facilities on Mainland Tanzania increased from 8,458 in 2022 to more than 10,000 in 2026.

Maternal mortality declined from 197 to 104 deaths per 100,000 live births, while newborn mortality fell from 25 to 19 deaths per 1,000 live births. Antenatal care coverage reached 98 per cent, and deliveries in health facilities increased from 83 per cent to 98 per cent.

In education, government financing rose from approximately 5.6tri/- in fiscal year 2022-23 to 6.3tri/- in 2025-26. The government has also continued providing fee-free basic education and opportunities for students who previously left school, including girls affected by pregnancy, to resume their studies.

Access to electricity has also expanded, with all 12,318 villages on Mainland Tanzania connected to the national grid and overall electrification reaching approximately 79.5 per cent.

Ulega also highlighted infrastructure development, including the operation of more than 700 kilometres of the Standard Gauge Railway and the Julius Nyerere Hydropower Project (JNHPP), which has an installed generation capacity of 2,115 megawatts.

Investments across productive sectors have generated more than 4.2 million employment opportunities, while the basic-needs poverty rate declined from 26.4 per cent in 2020 to 24.9 per cent in 2025.

Social protection has remained part of the government's efforts to support vulnerable households. "The Productive Social Safety Net supported approximately 1.36 million households, benefiting more than 5.1 million people," Mr Ulega said.

Access to clean water reached 85.2 per cent in rural areas and 92.5 per cent in urban areas, while internet penetration increased to 83.5 per cent, supported by investments in communications infrastructure and the national fibre-optic network.

The government also stressed that expanding digital connectivity must go hand in hand with privacy protection, online safety and measures to protect children.

Environmental initiatives featured in the presentation, including the production of more than 167 million tree seedlings during fiscal year 2025-26 and an increase in access to clean cooking from 15.9 per cent to 23.4 per cent.

Tanzania said the progress reflects its broader commitment to ensuring that human rights are not confined to legislation but are reflected in citizens' everyday lives.

The government reaffirmed its commitment to further reforms, stronger institutions and international cooperation, guided by Tanzania Development Vision 2050 and the principle of leaving no one behind.

CamScanner